JARIDA LA EASTC

JULAI - SEPTEMBA 2026



EASTC YASAINI MIKATABA YA USHIRIKIANO YA MoU NA MoA NA JOOUST

Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) kilisaini Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) pamoja na Mkataba wa Makubaliano (MoA) na Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia (JOOUST) cha nchini Kenya, kwa lengo la kuimarisha na kukuza ushirikiano katika maeneo ya taaluma, utafiti, ubunifu na machapisho ya kitaaluma.

Makubaliano hayo yalisainiwa na Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), Dkt. Tumaini Katunzi kwa niaba ya EASTC, pamoja na Prof. Emily Achieng Akuno,Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia (JOOUST), kwa niaba ya JOOUST. Hafla ya utiaji saini wa mikataba ya makubaliano ilifanyika katika Kampasi ya EASTC, Dar es Salaam, tarehe 11 Septemba 2026.

Akizungumza baada ya kusaini mikataba hiyo, Dkt. Katunzi alisema ushirikiano huo utafungua fursa mbalimbali katika maeneo ya utafiti, ubunifu na machapisho ya kitaaluma.

Aidha, alisema makubaliano hayo yatawezesha taasisi zote kufundisha baadhi ya programu kwa pamoja na kubadilishana uzoefu na utaalamu miongoni mwa wanataaluma wa EASTC na JOOUST.

Dkt. Katunzi alieleza kuwa EASTC ina ubobezi mkubwa katika maeneo ya takwimu rasmi na uchambuzi wa data, huku JOOUST ikiwa na ubobezi katika kilimo, sayansi na teknolojia. Alisema mikataba hiyo ni nyenzo muhimu ya kuunganisha utaalamu wa taasisi zote hasa katika takwimu za kilimo ambapo kwa sasa EASTC inashirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kufundisha programu hiyo.



Kwa upande wake, Prof. Emily Achieng' Akuno, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha JOOUST alisema kuwa JOOUST imebobea katika kilimo, Sayansi na Teknolojia na tafiti zinazohusu chakula, ushirikiano huo utaisaidia taasisi hiyo kuimarisha matumizi ya takwimu rasmi katika shughuli zake za utafiti.

Alisema ushirikiano kati ya JOOUST na EASTC utasaidia kuimarisha tafiti, sayansi na teknolojia, hususan katika matumizi na uchambuzi wa takwimu rasmi, jambo litakalosaidia kuzalisha maarifa na suluhisho lenye manufaa kwa jamii.



Dkt. Tumaini M. Katunzi
Mkuu wa Chuo, EASTC

Karibu katika Jarida la Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), kituo cha ubora katika mafunzo ya Takwimu Rasmi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

EASTC inaendelea kujikita katika kutoa elimu na mafunzo bora, kuimarisha utafiti na ubunifu, pamoja na kujenga uwezo wa wataalamu katika matumizi ya takwimu na data kwa ajili ya kufanya maamuzi yanayotegemea ushahidi na kuchochea maendeleo endelevu.

Kupitia ushirikiano wa kitaaluma na kitaalamu ndani na nje ya Afrika, tunaendelea kujenga jumuiya yenye ubunifu, maarifa na uwezo wa kuleta matokeo chanya katika jamii.
Karibu usome na kufahamu zaidi kuhusu shughuli, mafanikio na maendeleo mbalimbali ya EASTC katika kipindi hiki.

Katibu Mkuu MOEVT Atembelea Banda la EASTC

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Ndg. Khamis Abdulla Said alitembelea banda la Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) katika Maonesho ya Saba ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Unguja,kuanzia Julai 14-20 ,2026.

Ndg.Khamis alipongeza EASTC kwa ushiriki wake katika maonesho hayo na kwa mchango wake endelevu katika kutoa elimu na huduma za kitaalamu katika nyanja za takwimu, sayansi ya data na taaluma zinazohusiana.

Aidha alieleza kuwa ushiriki wa chuo katika maonesho hayo unatoa fursa kwa wanafunzi, wazazi na wadau mbalimbali wa elimu kupata taarifa sahihi kuhusu programu za masomo, udahili na huduma zinazotolewa na chuo.





MAADHIMISHO YA KILELE CHA MAONESHO YA SABA YA WIKI YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR 2026

Kaimu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mhe.Shaaban Ali Othman, Mgeni Rasmi katika kilele cha Maonesho ya Saba ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar alitembelea banda la Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) katika maonesho yaliyofanyika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Unguja Julai16, 2026.

Katika ziara hiyo, Makamu Mkuu wa Chuo Fedha, Mipango na Utawala Dkt. France Shayo, alimkaribisha Mhe.Waziri na kumpatia maelezo kuhusu programu mbalimbali za masomo zinazotolewa na EASTC, shughuli za utafiti pamoja na fursa za mafunzo zinazolenga kuandaa wataalamu mahiri katika nyanja za takwimu, sayansi ya data na taaluma nyingine zinazochangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

“ Akizungumza baada ya kutembelea banda la EASTC Mhe. Othman aliipongeza EASTC kwa kushiriki kikamilifu katika maonesho hayo na kwa kuendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaaluma na udahili kwa wanafunzi na wananchi kwa ujumla, hatua inayochangia kuongeza uelewa kuhusu fursa za elimu ya juu.

Aidha, katika hotuba ya ufunguzi wa maonesho hayo, Mgeni Rasmi alisisitiza umuhimu wa kuunganisha elimu ya juu na ubunifu ili kuzalisha wahitimu wenye uwezo wa kutatua changamoto za jamii na kuchochea maendeleo ya taifa

Pia, alizitaka taasisi za elimu ya juu kuimarisha tafiti na kufanya mapitio ya mitaala ili iendane na mahitaji ya sasa ya soko la ajira sambamba na kuwajengea wanafunzi ujuzi wa ubunifu, ujasiriamali na matumizi ya teknolojia za kisasa badala ya kuwaandaa kutegemea ajira pekee.

Alibainisha kuwa msisitizo huo unaendana na kaulimbiu ya mwaka huu, “Ubunifu na Taaluma ni Msingi wa Maendeleo,” akieleza kuwa elimu bora, tafiti na ubunifu ni nguzo muhimu katika kujenga uchumi shindani na maendeleo endelevu ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Kauli mbiu: “*Ubunifu na Taaluma ni Msingi wa Maendeleo*”.

Mkuu wa Mkoa; Asisitiza nafasi ya Takwimu Katika Maendeleo Ya Taifa.



Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Mhe. Mohammed Ali Abdalla alitembelea banda la EASTC Katika Maonesho ya Saba ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Unguja kuanzia Julai 14-20, 2026.Aidha, alipata fursa ya kujionea huduma mbalimbali zinazotolewa na chuo pamoja na kuzungumza na timu ya EASTC kuhusu ya nafasi ya takwimu katika maendeleo ya taifa na ukanda wa Afrika Mashariki.

Wanafunzi Wakihudumiwa Kwenye Banda La EASTC



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko Ndg.Samuel Marandu akiwahudumia wanafunzi waliotembelea banda la EASTC kutuma maombi ya chuo katika mfumo wa online application (OLAP) katika Maonesho ya Saba ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar 2026 yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Unguja, Zanzibar.

MATUKIO MBALIMBALI KATIKA WIKI YA ELIMU YA JUU (ZNZ)

Dkt. Tumaini Katunzi alishiriki katika Maonesho ya Saba ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar 2026

Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), Dkt. Tumaini Katunzi, alishiriki katika Maonesho ya Saba ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar 2026 yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Unguja, Zanzibar

Katika ziara hiyo, Dkt. Katunzi aliipongeza timu ya Masoko na Mawasiliano ya Chuo kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutoa huduma za ushauri wa kitaaluma kwa wanafunzi, wazazi na wadau mbalimbali wanaotembelea banda la EASTC, pamoja na kutangaza programu za masomo zinazotolewa na Chuo.



Aidha, Dkt. Katunzi alipata fursa ya kumkaribisha Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Prof. Henry Chalu, alipotembelea banda la EASTC na kujionea huduma mbalimbali zinazotolewa kwa wageni wa maonesho hayo.





> *Mhe.Balozi Coppola alisisitiza umuhimu wa kuimarisha elimu ya Takwimu katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ili kusaidia kufanya maamuzi sahihi yanayotegemea takwimu. Aidha alieleza ushirikiano kati ya EASTC, AICS na washirika wengine wa maendeleo ni hatua muhimu katika kujenga uwezo wa kitaalamu katika eneo hilo..”*

SUMMMER SCHOOL PROGRAMME

ITALIA YAIMARISHA USHIRIKIANO NA TANZANIA KUENDELEZA MAFUNZO YA TAKWIMU KUPITIA EASTC.

Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika, Dkt. Tumaini Katunzi, na Mgeni Rasmi, Balozi wa Italia nchini Tanzania, Mhe. Giuseppe Sean Coppola, walizindua mpango wa mafunzo ya muda mfupi (Summer School programme), unaotekelezwa chini ya mradi wa “Strengthening the EASTC’s Educational Offer in Statistics to Benefit Sub-Saharan African Countries”.

Hafla hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa EASTC, Dar es Salaam, mnamo Aprili 15,2026, na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali mashuhuri, akiwemo Mwakilishi Mkazi wa Italian Agency for Development Cooperation (AICS), Bw. Paolo Rizzini, wawakilishi kutoka Chuo cha Politecnico di Torino (POLITO), Prof. Roberta Fontana na Bi.Elizabeth Mascareus,Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Amina Msengwa, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Kikanda ya Chuo, pamoja na Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Bw. Salum K. Ali, Mwenyekiti wa EASTC Industrial Advisory Committee, Bw. Titus Mwisomba; pamoja na wageni wengine waalikwa na watumishi wa chuo.



Picha ya Pamoja ya mkuu wa chuo cha Takwimu mashariki mwa Afrika Dkt.Tumaini Katunzi, Bw.Paolo Rizzini, Mwakilishi wa shirika la maendeleo la AICS nchini Tanzania,Prof.Stephano Bonnini mtaalamu wa Takwimu na Sayansi ya Data kutoka Chuo kikuu cha Ferrara Italia,washiriki wa mafunzo na watumishi wa EASTC mara baada ya ufunguzi wa mafunzo ya muda mfupi (Summer School programme) kuhusu Multivariete Data Analysis and Data Mining in Applied Research yaliyofanyika katika kampasi ya EASTC Dar es Salaam, Julai 27,2026.



MAFUNZO YA MUDA MFUPI YA

Multivariete Data Analysis and Data Mining in Applied Research

Mwezeshaji wa mafunzo Prof. Stephano Bonnini kutoka Chuo Kikuu cha Ferrara Italia, akifundisha wataalamu wa takwimu kozi ya Multivariete Data Analysis and Data Mining in Applied Research yaliyofanyika katika darasa la data LAB EASTC, Dar es Salaam Julai 27,2026





Matukio mbalimbali katika mafunzo ya summer school program yaliyofanyika EASTC, Dar Es Salaam, Yakiongozwa na Wakufunzi kutoka Nchi Italia.



HOTUBA FUPI

Ufunguzi wa summer school programme



Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Italia AICS nchini Tanzania Bw. Paolo Razzini, akitoa hotuba fupi kwa washiriki wa mafunzo na watumishi wa EASTC wakati wa ufunguzi wa kozi ya Multivariate Data Analysis and Data Mining in Applied Research (summer school programme) iliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa EASTC, Dar es Salaam, Julai 27,2026.

MAFUNZO YA MUDA MFUPI YA

“Hidden Markov model for East African Time Series: Climate



Hydrology, Health and Society”

Mwezeshaji wa mafunzo Prof. Daniele Cappelletti kutoka idara ya sayansi za hisabati chuo kikuu cha Politecnico di Torino Italia, akiendesha mafunzo ya “Hidden Markov model for East African Time Series: Climate, Hydrology, Health and Society”, yaliyofanyika EASTC Dar es Salaam,tarehe 24 Agosti-04 Septemba 2026.

EASTC YAENDESHA MAFUNZO YA DEPENDENCE MODELS FOR RISK MANAGEMENT IN RELIABILITY, FINANCE AND ENVIRONMENTAL SCIENCES

Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), kinaendelea kutoa mafunzo kwa wataalamu wa takwimu nchini Tanzania kupitia programu mbalimbali za mafunzo ya kitaalamu, zinazolenga kuwajengea ujuzi na uwezo katika matumizi ya mbinu za kisasa za takwimu na uchambuzi wa data.

Mkuu wa Kitengo cha Mafunzo ya Muda Mfupi na Masomo kwa Njia ya Masafa,Bw. Nelson Ndifwa kwa niaba ya Mkuu wa Chuo, alifunga rasmi mafunzo ya muda mfupi ya "Dependence Models for Risk Management in Reliability, Finance and Environmental Sciences", yaliyofanyika chuoni EASTC, jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 7 hadi 18 Septemba 2026.

Katika hafla hiyo, Bw. Ndifwa aliwapongeza washiriki kwa kukamilisha mafunzo hayo na kuwatunuku vyeti vya ushiriki. Pia, aliwahimiza kutumia maarifa na ujuzi walioupata katika mafunzo hayo katika utekelezaji wa majukumu yao ya kitaalamu na tafiti. Aidha, aliwahimiza kujiunga na programu zinazoendelea kutolewa na Chuo.



Mafunzo hayo ni mwendelezo wa Summer School Programme yaliyotolewa na EASTC kwa kushirikiana na Politecnico di Torino (POLITO), kwa lengo la kuimarisha ujuzi na uwezo wa wataalamu katika maeneo mbalimbali ya takwimu, uchambuzi wa data na matumizi ya mbinu za kisasa katika tafiti.



Programu hiyo inafadhiliwa na Ubalozi wa Italia nchini Tanzania pamoja na Italian Agency for Development Cooperation (AICS), na inatekelezwa kwa ushirikiano wa wakufunzi mahiri kutoka Politecnico di Torino (POLITO), Italia.



Dkt.Iddi Haruna ahamasisha umuhimu wa kutunza na kuimarisha afya ya akili kwa watumishi wa EASTC

Mtalaamu wa afya ya akili kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Dkt.Iddi Haruna akitoa elimu kuhusu umuhimu wa kutunza na kuimarisha afya ya akili kwa watumishi wa Chuo cha Takwimu mashariki mwa Afrika (EASTC), wakati wa kikao cha kawaida cha watumishi kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano tarehe 04/09/2026.

Katika kikao hicho, watumishi walipata fursa ya kupima afya zao kama sehemu ya jitihada za kuhamasisha utunzaji wa afya na kuimarisha ustawi wao mahali pa kazi.



NIC yatoa elimu ya uwekezaji kwa watumishi wa EASTC

Bw.Octavian Lyimo ,kutoka shirika la Bima ya Taifa (NIC), akitoa elimu kwa watumishi wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), kuhusu fursa mbali mbali za uwekezaji,ikiwemo uwekezaji katika hati fungani za serikali (Treasury Bonds), pamoja na huduma za bima zinazotolewa na NIC, ikiwemo bima ya maisha yenye akiba.Elimu hiyo ilitolewa wakati wa kikao cha cha kawaida cha watumishi wa EASTC kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa chuo tarehe 4 Septemba 2026



Benki ya TCB yatoa elimu kwa watumishi EASTC kuhusu huduma mbali mbali za bima

Bw.Mulindwa Tishekwa,Meneja wa Tawi la Benki ya TCB,akitoa elimu kwa watumishi wa chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) kuhusu huduma mbali mbali za bima zinazotolewa na benki hiyo,zikiwemo bima ya maisha,bima ya ajali na bima ya nyumba.Elimu hiyo ilitolewa wakati wa kikao cha cha kawaida cha watumishi wa EASTC kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa chuo tarehe 4 Septemba 2026.

JUKWAA LA WADAU

EASTC YAENDELEA KUIMARISHA UWEZO WA WATAALAMU WATAKWIMU KUPITIA MAFUNZO YA KITAIFA YA R NCHINI BOTSWANA

Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) kimeendelea kuimarisha uwezo wa wataalamu wa takwimu kwa kutoa mafunzo ya kitaifa kuhusu matumizi ya programu ya R katika usimamizi, uchakataji na uchambuzi wa takwimu rasmi, yaliyofanyika nchini Botswana kuanzia tarehe 6 hadi 17 Julai 2026.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Mandeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na kutolewa na wataalamu kutoka EASTC kwa watumishi wa ofisi ya Takwimu Botswana pamoja na Benki Kuu ya Botswana (Bank of Botswana) yakilenga kuwawezesha kutumia mbinu za kisasa katika uzalishaji wa takwimu rasmi zenye ubora na zinazokidhi viwango vya kimataifa.

Akizungumza wakati wa hafla ya kufunga mafunzo hayo Naibu Mkurugenzi wa Takwimu Botswana Dkt. Lucky Mokgatle alitoa shukrani za dhati kwa Sekretarieti ya SADC kwa kuratibu mafunzo hayo na kwa EASTC kwa kutoa wataalamu wenye weledi wa hali ya juu. Aliwahimiza washiriki kutumia kwa vitendo maarifa na ujuzi walioupata katika shughuli zao za kila siku na kuendelea kushirikiana na wakufunzi wa EASTC wanapohitaji msaada wa kitaalamu.

Kwa upande wake mwakilishi wa Sekretarieti ya SADC Bw. Rajive Ajodhea alisisitiza umuhimu wa kuendelea kutumia programu ya R katika uzalishaji, uchakataji na uchambuzi wa takwimu rasmi. Alieleza kuwa matumizi endelevu ya programu hiyo ndiyo njia bora ya kudumisha ujuzi uliopatikana na kuongeza manufaa ya mafunzo hayo kwa taasisi zinazozalisha takwimu.



Naye Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) Dkt.Tumaini Katunzi, aliwapongeza washiriki wote kwa kukamilisha mafunzo hayo ya kina na kusisitiza kuwa programu ya R ni nyenzo muhimu ya wazi (open-source) inayowezesha uzalishaji wa takwimu rasmi zenye ubora, uwazi na zinazoweza kuhakikiwa kwa urahisi (reproducibility).

Aliwahimiza washiriki kuendelea kufanya mazoezi maarifa waliyojifunza na kuwajengea uwezo wenzao katika maeneo yao ya kazi. Aidha, alisisitiza dhamira ya EASTC ya kuendelea kuimarisha uwezo wa taasisi za takwimu barani Afrika kupitia mafunzo, tafiti, ushauri wa kitaalamu na programu za kitaaluma.

EASTC YAHITIMISHA AWAMU YA KWANZA YA MAFUNZO YA R SOFTWARE KWA NCHI WANACHAMA WA SADC

Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika (EASTC) kimehitimisha awamu ya kwanza ya mafunzo kwa watakwimu na watumishi wanaofanya kazi katika mifumo ya kitaifa ya takwimu kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

EASTC ilipewa jukumu na SADC la kuandaa na kutoa mafunzo ya “National Training on R Software in SADC Member States: Data Management, Processing, and Analysis for Official Statistics.” Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea washiriki ujuzi wa kutumia programu ya R katika usimamizi, uchakataji na uchanganuzi wa data kwa ajili ya uzalishaji wa takwimu rasmi.



Awamu ya kwanza ya mafunzo hayo imehusisha nchi tano ambazo ni Eswatini, Botswana, Zimbabwe, Madagascar na Msumbiji, ambapo Msumbiji imekuwa nchi ya tano na ya mwisho katika awamu hii.

Akizungumza katika hafla ya kufunga mafunzo hayo iliyofanyika jijini Maputo, Msumbiji, Makamu Mkuu wa Chuo – Mipango, Fedha na Utawala Dkt. France Shayo ameishukuru SADC kwa kukiamini Chuo na kukipa jukumu la kutoa mafunzo hayo kwa wataalamu kutoka nchi wanachama.

Dkt. Shayo aliwahimiza washiriki kutumia maarifa na ujuzi walioupata katika mafunzo hayo ili kuboresha kazi zao na kuchangia katika uzalishaji wa takwimu bora, sahihi na zenye kukidhi mahitaji ya nchi zao.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa SADC Bi. Zarafenosoa Ruth, ameishukuru EASTC kwa kutoa wataalamu wenye weledi waliowezesha utekelezaji wa mafunzo hayo kwa ufanisi.
Bi. Ruth alipongeza ushirikiano uliopo kati ya SADC na EASTC, akieleza kuwa mafunzo hayo ni sehemu muhimu ya kuimarisha uwezo wa wataalamu wa takwimu katika nchi wanachama wa SADC, hususan katika matumizi ya teknolojia na zana za kisasa za uchambuzi wa data.

Mafunzo ya “Leadership Training for SADC Statistics Committee”



Picha ya Pamoja ya wahadhiri kutoka Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) Dkt.Joyce Minja, Bi.Donatha Kemirembe na wakuu wa taasisi za Takwimu kutoka Nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), mara baada ya kukamilika kwa mafunzo ya “Leadership Training for SADC Statistics Committee” ,yaliyofanyika nchini Mauritius kwa ushirikiano kati ya EASTC,SADC na Office for National Statistics (ONS) ya Uingereza. Mafunzo hayo yalilenga kuimarisha uwezo wa viongozi wa wakuu wa Taasisi za Takwimu na kuwawezesha kuongoza mabadiliko chanya kwa ajili ya maendeleo ya mifumo ya takwimu na nchi zao.



Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), Dkt. Tumaini M. Katunzi aliongoza Kikao cha Kawaida cha Watumishi kwa Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2026/2027, kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa EASTC tarehe 4 Septemba 2026.

Lengo la kikao hicho lilikuwa ni kujadili masuala mbalimbali yanayohusu ustawi wa watumishi, uwajibikaji, mawasiliano, ushirikiano na ushirikishwaji wa watumishi katika shughuli na maendeleo ya Chuo.

MAFANIKIO YA WATUMISHI

Mkuu wa Chuo aliwatunuku vyeti vya pongezi watumishi waliohitimu masomo ya Shahada ya Uzamivu (PhD)

Dkt. Janeth Mchwampaka akipokea cheti cha pongezi kutoka kwa Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), Dkt Tumaini Katunzi, baada ya kuhitimu Shahada ya Uzamivu katika Hisabati (Doctor of philosophy in Mathematics-PhD).



Dkt. Sospeter Mchunguzi akipokea cheti cha pongezi kutoka kwa Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), Dkt Tumaini Katunzi, baada ya kuhitimu Shahada ya Uzamivu katika usimamizi (Doctor of philosophy in Management -PhD)



MAFANIKIO YA WANAFUNZI

BoT NA EASTC WAENDESHA MAFUNZO KWA VITENDO KWA WANAFUNZI WA SAYANSI YA DATA

Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) Dkt. Tumaini M. Katunzi, aliambatana na Makamu Wakuu wa Chuo, kutembelea na kukagua maendeleo ya Mafunzo kwa Vitendo (Industrial Training) yaliyotolewa kwa wanafunzi wanaosoma Sayansi ya Data (Data Science) katika Kampasi ya EASTC Changanyikeni, Dar es Salaam.

Mafunzo hayo yalitekelezwa kwa ushirikiano kati ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na EASTC, yakilenga kuwawezesha wanafunzi kutumia kwa vitendo maarifa na ujuzi walioupata katika Nyanja za Sayansi ya Data (Data Science) na Akili Unde (Artificial Intelligence) katika kubuni na kuedeleza bunifu zitakazosaidia suluhisho la kukabiliana na changamoto halisi za kiuchumi na kijamii

Aidha, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ikiwa ni mdau muhimu wa kimkakati, ilishiriki kuratibu na kubainisha maeneo ya kipaumbele yenye changamoto halisi ambayo wanafunzi waliyafanyia kazi kwa kutumia teknolojia za kisasa za uchambuzi wa data na Akili Unde.

Dhamira ya EASTC ni kutoa elimu na mafunzo yenye ubora yanayozingatia mahitaji ya soko la ajira na kuwawezesha wanafunzi kujenga ujuzi wa vitendo, ubunifu na uwezo wa kushindana katika mazingira ya kazi yanayobadilika kwa kasi.

Katika kutekeleza dhamira hiyo, ushirikiano kati ya EASTC na taasisi za kimkakati, ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania (BoT) unaendelea kuwa chachu muhimu katika kuimarisha uhusiano kati ya elimu na mafunzo ya kitaaluma na mahitaji halisi ya sekta mbalimbali.



MAONESHO YA NANENANE 2026

NAIBU WAZIRI WA KILIMO AHIMIZA WANANCHI KUTUMIA FURSA YA MAONESHO YA NANENANE KUJIFUNZA NA KUPATA MASOKO

Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David E. Silinde (MB) ambaye alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa Maonesho ya Wakulima na Wafugaji (Nanenane) Kanda ya Kaskazini yaliyofanyika katika Viwanja vya Themi - jijini Arusha, aliwataka wananchi na wadau mbalimbali kuendelea kutembelea mabanda ya maonesho ili kujifunza teknolojia mbalimbali, kubadilishana uzoefu na kujionea fursa zilizopo katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mhe. Silinde alisema maonesho ya Nanenane ni jukwaa muhimu la kujifunza, kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa na kujenga masoko ya uhakika kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.

“Ni muhimu kutambua soko kabla ya kuanza uzalishaji; hiyo ndiyo dunia ya sasa. Unaangalia soko kabla ya kwenda shambani,” alisema Mhe. Silinde.

Alitoa kauli hiyo wakati akifungua rasmi Maonesho ya Wakulima na Wafugaji (Nanenane) kanda ya kaskazini, ambapo alihimiza wananchi kutumia kikamilifu maonesho hayo.

Katika Maonesho hayo yaliyoanza Agosti 01-08, 2026, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), kilishiriki kwa kutoa elimu na huduma ya udahili wa programu za shahada, Stashahada, Astashahada na Shahada za umahiri (Master’s Degree), msaada wa kutumia mfumo wa maombi ya udahili (online Application),kutoa mwongozo wa vigezo na sifa za kujiuga na programu za chuo,kutoa taarifa kuhusu ada za masomo, ufadhili na fursa za scholarship,pamoja na kutoa ushauri kuhusu programu za Takwimu,Sayansi ya Data (Data Science) na fursa za ajira.

Ushiriki wa EASTC ulilenga kuwafikia wanafunzi, wazazi na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu na wananchi kwa ujumla ili kuwapatia taarifa sahihi kuhusu programu mbalimbali za masomo zinazotolewa na Chuo.





Makamu mkuu wa Chuo Taaluma,tafiti na Ushauri wa Kitaalamu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), Dkt.Indiael Daniel Kaaya alishiriki katika maonesho hayo na kuwahimiza timu ya masoko kuendelea kutoa taarifa sahihi za programu za masomo zinazotolewa na chuo pamoja na kuendelea kutoa elimu na ushauri wa kitaalamu kwa wanafunzi, wazazi na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu wanaotembelea banda la chuo.

Aidha,Dkt.Kaaya alipata fursa ya kutembelea baadhi ya mabanda ya Taasisi za elimu zilioshiriki katika maonesho, ikiwemo taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Chuo kikuu cha katoliki Mwenge (MWECAU) kujionea huduma mbali mbali zinazotolewa.

Maonesho hayo yaliongozwa na kauli mbiu isemayo"Tambua soko;Ongeza Tija kutekeleza Dira 2050"





DKT. KATUNZI AIISHIRIKI WIKI YA KITAIFA YA ELIMU, UJUZI NA UBUNIFU.

Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) Dkt. Tumaini M. Katunzi alishiriki katika Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu 2026 yaliyofanyika kuanzia tarehe 15-24 Agosti 2026, katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Usagara, jijini Tanga.

Maadhimisho hayo yalifuguliwa rasmi na Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe.Prof Adolf Mkenda,yakilenga kuhamasisha na kuonesha mchango wa ujuzi na ubunifu katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Dkt. Katunzi aliwapongeza maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko kwa kazi kubwa wanayoifanya kutoa huduma za ushauri wa kitaaluma kwa wanafunzi, wazazi na wadau mbalimbali wanaotembelea banda la EASTC pamoja na kutoa taarifa kuhusu programu mbalimbali za masomo zinazotolewa na Chuo.

Aidha, Dkt. Katunzi alisisitiza umuhimu wa EASTC kuendelea kutumia maonesho hayo kama fursa ya kuifikisha elimu ya takwimu kwa jamii,kuwaelimisha wadau kuhusu nafasi ya takwimu katika malengo ya Dira ya Maendeleo ya taifa 2050 na kuwahamasisha wanafunzi kujiunga na programu mbalimbali zinazotolewa na Chuo.

Maonesho hayo yaliongozwa na kaulimbiu isemayo: “Elimu, Ujuzi, Ubunifu, Njia ya Kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.” yalitoa fursa ya kwa taasisi mbali mbali za elimu,wadau wa sekta ya elimu, wanafunzi, wazazi na Wananchi kujifunza na kubadilishana uzoefu katika maendeleo ya elimu,ujuzi na ubunifu nchini.



Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), Prof. Ahmed M. Ame, aliongoza wajumbe wa Bodi ya Ushauri wa Chuo pamoja na Menejimenti ya Chuo kutembelea na kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa Jengo la Taaluma kupitia Mradi wa Higher Education for Economic Transformation (HEET).

Wajumbe walipata fursa ya kujionea hatua za utekelezaji wa mradi huo na maendeleo yaliyofikiwa hadi sasa.

Ziara hiyo ilifanyika kabla ya kufanyika kwa kikao cha Bodi ya Ushauri ya Chuo (Ministerial Advisory Board) kwa robo ya nne ya mwaka wa fedha 2025/2026, kilichofanyika Agosti 21,2026, katika ukumbi wa mikutano wa EASTC.

Bodi ilipongeza juhudi za Menejimenti ya Chuo katika kusimamia utekelezaji wa mradi huo huku ikisisitiza umuhimu wa kuendelea kuzingatia ubora, uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali ili kuhakikisha miradi yote inakamilika kwa wakati



EASTC ILIENDESHA KIKAO CHA KAMATI YA UKAGUZI ROBO YA NNE YA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi ya Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) Dkt. Maulid J. Maulid ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), aliongoza Kikao cha Kamati ya Ukaguzi ya EASTC kwa Robo ya Nne ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 kilichofanyika tarehe 14 Agosti,2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa EASTC,Jijini Dar es Salaam.

Lengo la kikao hicho ni kupitia na kujadili masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi wa fedha, mifumo ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa rasilimali za chuo, pamoja na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi.

EASTC PROGRAMES

1 MASTERS PROGRAMES

- Master Degree in Official Statistics (MOS)
- Master of Science in Agricultural Statistics (In collaboration with Sokoine University of Agriculture-SUA)
- Master Degree in Monitorig and Evaluation with Statistics (MMES)
- Executive Master Degree in Official Statistics (MOS)
- Executive Master of Monitoring and Evaluation with Statistics (EMMES)

2 UNDERGRADUATE PROGRAMES

- Bachelor Degree in Official Statistical (BOS)
- Bachelor Degree in Data Science (BDS)
- Bachelor Degree in Business Statistics and Economics (BBSE)
- Bachelor Degree in Agricultural Statistics and Economics (BASE)
- Bachelor of Science in Actuarial Statistics (BSAS)
- Bachelor Degree in Digital Economics and Statistics (BDES)

3 CERTIFICATE AND DIPLOMA PROGRAMES

- Basic Technician Certificate in Statistics (BTCST)
- Basic Technician Certificate in Information Technology (BTCIT)
- Ordinary Diploma in Statistics (ODS)
- Ordinary Diploma in Information Technology (ODIT)



Tel: General +255 22 2925000 | +255 735 784 106

Rector's Direct Line +255 784 784 106

E-mail: info@eastc.ac.tz | rector@eastc.ac.tz

Website: http://www.eastc.ac.tz

P.O.BOX 35103-Dar es Salaam Tanzania